**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA**
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)*

Simu

2 Barabara ya Bomani
S.L.P 1490,
Baruapepe: **td@nanyambatc.go.tz** **63682 NANYAMBA-MTWARA**

# TANGAZO LA KUPATA WAZABUNI WA VIFAA VYA UJENZI

## KATIKA HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA

Halmashauri ya Mji Nanyamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepokea fedha kwaajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Shule Katika Shule ya Sekondari Mpya Mtiniko na Shule ya Sekondari Namtumbuka kwa ajili ya Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa, Jengo la Utawala, Maabara, Maktaba, Chumba Cha Tehama, Kichomea taka, Tenki la Maji Ardhini, Matundu ya Vyoo na Nyumba ya Walimu (2 in 1) Kupitia Mradi wa SEQUIP.

Baadhi ya vifaa vya ujenzi vinavyohitajika ni kama ifuatavyo.

| Na. | JINA LA KIFAA |
|---|---|
| 1 | Nondo, Misumari na wire Mesh |
| 2 | Mbao |
| 3 | Vifaa vya dari (gypsum boards, Pvc etc) |
| 4 | Rangi na Vifaa vya Umaliziaji |
| 5 | Marumaru |
| 6 | Mabati, Kofia na Misumari ya Bati |
| 7 | Vifaa vya Umeme na Maji |
| 8 | Madirisha ya Chuma na Vioo |
| 9 | Fremu za Milango na Shata za Milango |
| 10 | Vitasa na Bawaba |
| 11 | Saruji |

Hivyo, **Mkurugenzi Wa Mji Nanyamba** anawatangazia Wananchi, Wazabuni na Wasambazaji wa Vifaa/bidhaa wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kusambaza vifaa vya Ujenzi ambavyo vitatumika kujenga Majengo yaliyoainishwa hapo juu.

**Sifa na masharti kwa Wananchi, Wasambazaji na Wazabuni wanaohitajika ni kama ifuatavyo:-**

1) Muombaji **lazima** awe leseni ya biashara ya bidhaa husika na awasilishe nyaraka zifuatazo:
   a) Nakala ya Leseni ya Biashara
   b) Cheti cha Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN)
   c) Cheti cha usajili wa 'BRELA'
   d) Barua inayoonesha kwamba bei ya vifaa vya ujenzi alivyojaza hazitabadilika kwa muda wa miezi sita (06)
   e) Barua ya maombi ikitaja vifaa vya ujenzi anazoomba
   f) Wasifu wa kampuni (Company Profile)

2) Muombaji **lazima** awe na uwezo wa Kupeleka Vifaa hadi eneo la Ujenzi
3) Muombaji **lazima** awe uwezo wa Kutoa Risiti ya ki-eletroniki (EFD/EFR)
4) Malipo yote yatafanyika Kupitia Benki
5) Uchambuzi wa Maombi utafanyika kulingana bei halisi ya soko kwa kila kifaa kinachohitajika katika mradi, na siyo ujumla wa vifaa vilivyopo kwenye hati msako (quotation)
6) Muombaji atakayeshinda kuleta vifaa vya Ujenzi **lazima** asaini mkataba/makubaliano kabla ya kuleta vifaa alivyoshinda
7) Hati Msako / Nukuu za Bei (Quotation) zinapatikana kwenye Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi na Shule ya Sekondari Namtumbuka kwa Tzs. 20,000.00 kwa kila **Lot.**
8) Malipo ya Kablasha la Nukuu ya Bei yatafanyika katika Ofisi ya **Mkurugenzi wa Mji.** Waombaji wote wapitie Ofisi Na. 18 kwa maelekezo
9) Inasisitizwa kuwa waombaji lazima wajaze bei ya Vifaa vya Ujenzi na Malipo yatafanyika baada ya Vifaa hivyo kupokelewa katika eneo la Ujenzi

10) Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono kupitia **Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi na Shule ya Sekondari Namtumbuka kwa Anuani zifuatazo**

**MKUU WA SHULE,**

**SHULE YA SEKONDARI MTIMBWILIMBWI,**

**S.L.P 1490,**

**NANYAMBA – MTWARA.**

NA

**MKUU WA SHULE,**

**SHULE YA SEKONDARI NAMTUMBUKA,**

**S.L.P 1490,**

**NANYAMBA – MTWARA.**

*Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 31/07/2023 saa 3:30 Asubuhi na ndiyo siku ya ufunguzi.*

**Tangazo hili Limetolewa na:**

***MKURUGENZI MTENDAJI,***

***HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA***

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI
S. L. P 1490
NANYAMBA